

Shairi la "Pole Sana" liliandikwa na Mshairi Marehemu Hamidu Tambwe miaka Mwsihoni mwa mwaka 1969, likikusudiwa kama barua kwa Abuu Athumani Kapalata Mwaijumba wa Mbeya Tanzania.

POLE SANA

- | | |
|--|---|
| <p>1. Pole kaka zije mbio, akhi wangu mfadhili
Pole nakupa mwenzio, zisizo na tamthili,
Pole kaka mambo hayo, yasikuzushe akili,
Na tumuombe Jalali, kulikidhi azimio.</p> | <p>5. Pole adha iondoke, ubakiwe na shughuli,
Pole na yote makeke, yote yaende twawili,
Pole na uneemeke, kwa naimu na amali,
Na tumuombe Jalali, kulikidhi azimio.</p> |
| <p>2. Pole tuombe nasaha, kwa mambo hayo anzali,
Pole tuwe nayo siha, katika yetu miili,
Pole na pia buraha, iisighibu kwenda mbali,
Na tumuombe Jalali, kulikidhi azimio.</p> | <p>6. Pole usiwe na shaka, mambo hayo yahimili,
Pole siku itafika, atarudia kivuli,
Pole huko atakaa, ili azuru wa pili,
Na tumuombe Jalali, kulikidhi azimio.</p> |
| <p>3. Pole na tuendeleo, kutabahari kamili,
Pole sana tuijue, lugha yetu Kiswahili,
Pole ijapo ukae, izara kana sabili,
Na tumuombe Jalali, kulikidhi azimio.</p> | <p>7. Pole na hii jinai, isizushe sili sili,
Pole lake jitimai, aliondoshe Jalali,
Pole uwepouhai, mzuri kama asali,
Na tumuombe Jalali, kulikidhi azimio.</p> |
| <p>4. Pole tashwishi ighibu, hasa kwa wewe rijali,
Pole uwe mahabubu, uendele na shuli,
Pole pasina taabu, izidi yako akili,
Na tumuombe Jalali, kulikidhi azimio.</p> | <p>8. Pole nitue mwenzio, silete kisili sili,
Pole akhi kama hiyo, ijiri kwa kiadili,
Pole tanabahi hayo, ikiwa siyo dhalili,
Na tumuombe Jalali, kulikidhi azimio.</p> |

***Hamidu R Tambwe**
MBEYA
Sept. 1969.*
